TANZANIA APPLIED SPORTS AND EXERCISE PSYCHOLOGY ASSOCIATION
TASEPA
"Mindset Shapes Perfomance"

**Tanzania Applied Sports and Exercise Psychologists Association**
**S.L.P 60336, DAR ES SALAAM**
**Email: tasepatz1@gmail.com| Phone: 0754 773 275**
https://tasepa2.netlify.app/.
**Tabata, Ngorongoro Street**

## NA SAJINI TAJI ALPHONCE FELIX SIMBU ( Bingwa wa dunia wa MBIO za Marathon October 2025, zilizofanyika TOKYO JAPAN)

## BAADA YA KUSHINDA MBIO ZA MARATHON NCHINI JAPAN, SIMBU ALIKUA NA HAYA Y KUSEMA KWA VYOMBO VYA HABARI

Kwanza kabisa, namshukuru Mungu Mwenyezi kwa kuniwezesha kupata afya, nguvu na nafasi hii ya kufanikisha mafanikio haya.

Natoa shukrani za dhati kwa Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuunga mkono michezo na majeshi yetu.

Vilevile, namshukuru kwa dhati Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Jacob John Mkunda, na Mkuu wa Tawi la Mafunzo, Jenerali Mhona, kwa uongozi wao imara na hamasa kubwa.

Natoa shukrani maalum kwa mlezi wa timu ya riadha, Meja Jenerali Mbindi, Mkurugenzi wa Utimamu wa Mwili, Michezo na Utamaduni pamoja na timu yake yote, Kamanda wa Kikosi, na wanakikosi wenzangu wote wa 977 KJ.

Nawashukuru kwa dhati kocha wangu, meneja wa timu, pamoja na wenzangu wanariadha kwa ushirikiano wao mkubwa.

Kwa familia yangu ninayowapenda — asanteni kwa maombi, upendo na msaada wenu wa hali na mali ambao umekuwa nguzo yangu kuu.

Ninatoa shukrani kwa viongozi wa Shirikisho la Riadha Tanzania (Athletics Tanzania), Baraza la Michezo la Taifa (BMT), na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa sapoti yao ya dhati na imani waliyonionyesha.

Kwa Watanzania wote, kwa vyombo vya habari, na kwa mashabiki wangu popote walipo — asanteni sana kwa kuniamini, kunitia moyo na kunivumilia katika safari hii. Mafanikio haya ni matokeo ya juhudi, nidhamu, mshikamano, na maombi yenu.

Pia napenda kutoa shukrani za pekee kwa Chama cha Wanasaikolojia wa Michezo na Mazoezi Tanzania (TASEPA) kwa weledi na ushauri wao wa kisaikolojia ambao umenijenga kwa kiasi kikubwa. Kwa muda wote tangu nilipopata huduma yao, nimekuwa na mtazamo chanya, maono mapana, na kujiamini kila ninaposhindana. Ushirikiano wao umechangia sana mafanikio yangu ya kisaikolojia na kimchezo.

Felix
…………………………….. ……………………………
**ALPHONCE FELIX SIMBU** **Stamp**

TANZANIA APPLIED SPORTS AND EXERCISE PSYCHOLOGY ASSOCIATION
DATE 16/10
DAR-ES-SALAAM, TANZANIA